

Tafsiri za Riwaya za Kigeni kwa Kiswahili nchini Tanzania

Flavia Aiello Traore

Ikisiri

Makala hii inazingatia tafsiri ya kifasihi nchini Tanzania enzi za baada ya kujipatia uhuru. Inaeleza baadhi ya mbinu zilizotumiwa na wafasiri wa Kiswahili wakati wakishughulika na kazi za fasihi ya kigeni, hususani jinsi ya kukabiliana na vipengele vya kiutamaduni vya lugha chanzi kama vile kaida za kiutamaduni, misemo, methali n.k. Kwa ajili ya mada hii umechaguliwa mkusanyiko wa tafsiri nne zilizofanywa na Watanzania, yaani *Shamba la Wanyama* (Fortunatus Kawegere, 1967; tafsiri ya *Animal Farm*, cha Orwell, 1945), *Shujaa Okonkwo* (Clement Ndulute, 1973; tafsiri ya *Things Fall Apart*, cha Achebe, 1958), *Mzee na Bahari* (Cyprian Tirumanywa, 1980; tafsiri ya *The Old Man and the Sea*, cha Hemingway, 1952) na *Jambo la Maana* (Ebrahim Hussein, 1982; tafsiri ya hadithi tatu za Hans Christian Andersen: *The Emperor's New Clothes*, 1837, *Something*, 1858 na *The Old Street Lamp*, 1847).

1.0 Utangulizi

Tafsiri ni shughuli kongwe sana na wasomi wengi duniani walijitahidi kufafanua dhana hii na vipengele vyake vingi, hadi siku hizi ambapo imetambuliwa kama taaluma mahususi. Kutafsiri, yaani kutoa ujumbe au mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha chanzi au asili hadi lugha pokezi au lengwa, ni kazi ngumu na yenye utata. Kwa hakika ni uhamisho si wa maneno pwekepweke tu, bali wa miundo na maana za matini maalum ambazo haziwezi kueleweka vyema bila kujua tofauti za kiisimu za lugha zinazohusika, na vilevile tofauti zake za kitamaduni zinazompatia mfasiri matatizo makubwa zaidi (Mwansoko, 1996: 30). Ndiyo sababu tafsiri, hususani ya kifasihi, ambayo ina sifa zake pekee kutokana na matini zinavyopangiliwa kisanii (Mwansoko, 1996: 42), ni changamoto kubwa kwa wafasiri wote. Kuhusiana na jambo hili, Wamitila (2003: 211) pia anaeleza kuwa “kwa kuwa lugha hutofautiana kisauti, msamiati, muundo wake, nahau na misemo yake, huwa sio rahisi kuipata tafsiri inayolandana kabisa na kazi asili. Huu ndio msingi wa msembo wa Kiitaliano kuwa wafasiri ni wasaliti [*traduttori traditori*]”.

Makala hii inazingatia tafsiri ya kifasihi nchini Tanzania kwa upande wa maandishi ya kinathari. Makala yenyewe inachambua jinsi wafasiri walivyotafsiri kwa Kiswahili baadhi ya hadithi na riwaya za kigeni. Tafsiri ya kifasihi kwa Kiswahili ina historia ndefu, kuanzia na *Hamziya* na tenzi kadhaa zilizotokana na ushairi wa Kiarabu (Mazrui, 2007: 124). Shughuli ya kutafsiri kazi za kifasihi zilizoandikwa kwa lugha za Kiulaya ilianza wakati wamishenari na wakoloni

walipotafsiri kwa Kiswahili Biblia na vitabu vingi vya Kizungu (Bertoncini na wenz. 2009: 30-31). Enzi za baada ya nchi za Afrika Mashariki kujipatia uhuru tafsiri imetambuliwa kuwa ushahidi wa ubora wa Kiswahili. Mwalimu Nyerere, aliyekuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifungua njia kwa kutafsiri tamthilia mbili za William Shakespeare, yaani *Julius Caesar* (1599; *Juliasi Kaizari* 1964 na *The Merchant of Venice* (1596; *Mabepari wa Venisi* 1969), kwa ukamilifu na kwa kutumia ushairi na Kiswahili fasaha, kinyume na tafsiri zilizotangulia ambazo zilikuwa vifupisho vya kinathari tu.¹ Kazi yake iliwapa moyo wafasiri wengine kutafsiri fasihi ya kigeni kwa Kiswahili. Aidha, nchini Tanzania tafsiri za vitabu vya kigeni kwa Kiswahili zilionekana kuwa ni chombo cha ziada – cha msingi ni kazi za ubunifu – cha ukuzaji wa fasihi ya kisasa ya Kiswahili (Ruhumbika, 1983: 254).

Lengo la makala hii ni kufafanua mbinu zilizotumiwa na wafasiri Watanzania katika kutafsiri kazi za kigeni kwenda lugha ya Kiswahili. Kwa ajili ya kupambanua na kulinganisha mitindo ya kutafsiri ya wafasiri, nitahusika sana na utofautishaji wa mikakati miwili ya kitafsiri, yaani: (i) kuambatana sana na matini chanzi na kuhifadhi vipengele vyake vingi vya lugha na utamaduni ambavyo vitaonekana kama vigeni kwa wasomaji wa lugha lengwa; (ii) kuhamisha matini chanzi kwenye lugha na utamaduni wa lugha lengwa. Kwa namna hiyo, wasomaji wataona kazi ya tafsiri kama ya kienyeji. Wataalam wengi waliainisha mikakati hii, wakiwamo Lawrence Venuti (1995) aliyetumia kwa Kiingereza dhana za *foreignisation* na *domestication*, na Umberto Eco (2003) ambaye aliunda kwa Kiitaliano istilahi za *xenofilizzazione* na *localizzazione*. Utofautishaji huu kwa kiasi kikubwa unakaribiana na ule ulioelezwa na Mwansoko (1996: 26-27) baina ya tafsiri ya kisemantiki, ambayo inaegemea sana kwenye matini chanzi, na tafsiri ya mawasilino, ambayo inazingatia sana na kumlenga msomaji wa lugha lengwa.

Makala itatumia tafsiri nne zilizofanywa na wafasiri Watanzania, nazo ni: *Shamba la Wanyama* (Fortunatus Kawegere, 1967), *Shujaa Okonkwo* (Clement Ndulute, 1973), *Mzee na Bahari* (Cyprian Tirumanywa, 1980) na *Jambo la Maana* (Ebrahim Hussein, 1982). Makala yenyewe imegawanyika katika sehemu tatu: utangulizi, mjadala wa tafsiri husika na mwisho ni hitimisho. Katika mjadala kila kazi ya tafsiri iliyotajwa hapo juu itapewa nafasi yake stahiki. Mifano kadhaa itaonyeshwa kwa kueleza na kulinganisha mikakati ya wafasiri hawa, hususani namna walivyokabiliana na vipengele vya kitamaduni vya lugha chanzi, yaani lugha za jamii zenye maisha, dini, misemo, nahau na methali tofauti na yao.

¹ Kwa mfano katika mkusanyo wa *Hadithi Ingereza* uliochapishwa mwaka 1900 na UMCA nchini Zanzibar kulikuwa na vifupisho vya tamthilia za Shakespeare zikiwamo *The Taming of the Shrew* (Mwanamke Aliyefugwa), *The Tragedy of King Lear* (Baba na Binti) na *The Merchant of Venice* (Kuwia na Kuwiwa) (Mazrui, 2007: 133).

2.0 Tafsiri za Riwaya Husika

2.1 *Shamba la Wanyama* (Kawegere, 1967) Tafsiri ya *Animal Farm* (Orwell, 1945)

Animal Farm ni riwaya fupi iliyoandikwa na George Orwell. Huyu ni mwandishi na mwanahabari Mwingereza. Riwaya hii ni istiaara ya kihistoria ambapo wanyama wanaishia kuchukua madaraka katika shamba la binadamu, Bw. Jones. Kazi hii inawakilisha mapinduzi yaliyofanyika huko Urusi mwaka 1917. Ingawa Orwell alikuwa ni msoshalisti, aliona kwa wasiwasi kuwa Stalin na viongozi wenzake walianzisha udikteta. Fortunatus Kawegere alitafsiri mwanzo wa riwaya hiyo kama ifuatavyo:

Mr. Jones, of the Manor farm, had locked the hen-houses for the night, but was too drunk to remember to shut the pop-holes. With the ring of light from his lantern dancing from side to side he lurched across the yard, kicked off his boots at the back door, drew himself a last glass of beer from the barrel in the scullery, and made his way up to bed, where Mrs Jones was already snoring (uk. 1).

Shamba Ibura lilikuwa mali ya Bwana Mtiki. Siku moja alipokuwa amelewa sana alighafilika kufunga zizi baada ya kufunga kibanda cha kuku. Alijinywea bilauri yake ya mwisho, alivua viatu halafu akajitupa kitandani ambamo mkewe alikuwa ameishaanza kukoroma (uk. 7).

Mfano huu unadhihirisha wazi kwamba Kawegere katika kazi yake ya kutafsiri alihamisha kwa kiwango kikubwa matini chanzi kwenye lugha na utamaduni wa lugha lengwa ili wasomaji wasome na wafumbue kazi hii kama hadithi ya Kiswahili. Tabia yake ya “kuhamisha nyumbani” riwaya hii inatekelezwa kwa mbinu zifuatazo:

- Kubadilisha mahali: Manor Farm imekuwa Shamba Ibura, yaani mtaa wa mjini Bukoba alikozaliwa mfasiri, nchini Tanzania.
- Kubadilisha majina: Bw. Jones ameitwa Bwana Mtiki. Hata majina ya wahusika wengine wa riwaya hii yamebadilishwa, kwa mfano nguruwe Snowball amekuwa Mzushi, na mwenzake Napoleon alipata jina la Mkimwa. Hapa Kawegere alifuata mwenendo wa waandishi wengi wa Kiswahili, kuanzia na Shaaban Robert, yaani kutumia majina ya wahusika kwa kuakisi sifa na tabia zao (Wamitila, 1999: 35). Kutokana na mtazamo wa mfasiri, hulka za wanyama hawa ni mbaya sana; hata moyo wa Snowball, ambaye katika *Animal Farm* si mhusika mwovu kikamilifu, kwa kuwa amechorwa kama mtaalamu anayejali maisha ya wenzake, lakini baadaye anafukuzwa na dikteta Napoleon.
- Kuondoa maneno ya kitamaduni ya Kiingereza: mara nyingi mfasiri anafuta msamiati huu bila kutafuta visawe au maelezo, kwa mfano hapo juu maneno kama *beer* (bia), *barrel* (pipa la bia) na *scullery* (chumba karibu na

jiko cha kuhifadhi vyombo vya nyumbani) hayakutafsiriwa kabisa. Mfasiri pia alifuta *Mid summer's eve* (uk. 11; siku ya sherehe ya Waingereza inayoitwa pia siku ya Yohana Mtakatifu, tarehe 24 mwezi wa sita), na mifano mingineyo mingi.

- Mkakati mwingine wa Kawegere ni kuingiza maneno ya kijumla mahali pa maneno ya kitamaduni ya Kiingereza, kwa mfano tafsiri za *Brussels carpet* na *the lithograph of Queen Victoria* (uk. 14) imekuwa “mikeka iliyorembeshwa” na “picha kubwa” (uk. 23).
- Katika sehemu nyingine za riwaya mfasiri anaongeza misemo na nahau za Kiswahili hata kama hakuna msemu/nahau katika matini chanzi. Kwa mfano, katika ukurasa 19 sentensi ya *Mollie agreed, but she did not sound very convinced* ilitafsiriwa “Mjinga alikubali shingo upande”.

Kadhalika, mfasiri anaandika upya baadhi ya aya za riwaya hii. Kawegere, ambaye mwenyewe ni mwandishi wa hadithi na mashairi, kwa ujumla amefuta au amezibadilisha sana sentensi nyingi za matini chanzi, kama ambavyo inaonekana katika mfano wa hapo juu. Mkabala wa kitafsiri wa Kawegere pengine unaweza kuhusishwa na utamaduni wa fasihi simulizi, kwa kuwa mtambajii ni mbunifu anayeweza kuongeza, kurudia, kuondoa au kubadilisha vipengele fulani vya hadithi kulingana na vionjo vyake ili wasikilizaji wavutiwe navyo (Okpewho, 1992: 33).

Mfano mwingine wa mtindo wa Kawegere ni tafsiri ya wimbo wa “Beasts of England” ambao kwa mara ya kwanza uliimbwa na Askari Mzee (Old Major):

Beasts of England, beast of Ireland,	<i>Ndugu zangu e wanyama,</i>
Beasts of every land and clime,	<i>Mlio karibu hapa,</i>
Hearken to my joyful tidings	<i>Habari nzuri sikiliza,</i>
Of the golden future time...	<i>Siku moja itafika....</i>

Rings shall vanish from our noses,	<i>Siku hiyo ya furaha,</i>
And the harness from our back,	<i>Hazama zitakwisha,</i>
Bit and spur shall rust forever,	<i>Lijamu na kigwe pia,</i>
Cruel whips no more shall crack (uk.7).	<i>Vitatumiwa wanyama (uk. 14).</i>

Hapo mfasiri alichagua kubadilisha sana wimbo, si kwamba alifuta mahali kama “England” na “Ireland” tu, bali alichagua kutotafsiri maneno mengi, yakiwamo “cruel whips” (viboko vibaya) ambavyo ni ishara kuu ya utumiaji wa nguvu na mateso wakati wa ukoloni katika kumbukumbu za historia za watu wa Afrika. “Usahaulifu” huu unaweza kuhusishwa na mtazamo wa kiitikadi wa Kawegere ambaye hakukusudia kitabu cha *Shamba la Wanyama* kisomwe kama istiyari ya utawala wa ukoloni, bali alitaka hadithi hii ifasiriwe kama fumbo la kisiasa lililowasilisha wasiwasi wake kuhusu mapinduzi ya nchini kwake, yaani mapinduzi ya Unguja ya mwaka 1964, na kwa jumla kuhusu mipango ya Ujamaa.

Mfasiri mwenyewe alieleza katika mahojano na A. Mazrui kwamba kazi yake ya tafsiri ilichangiwa na *United States Information Service* (2007: 138). Kutokana na hayo yote, si jambo la kushangaza kuwa tafsiri hii ilichapishwa nje ya Tanzania, yaani mjini Nairobi na *East African Publishing House*.

2.2. Shujaa Okonkwo (Ndulute, 1973) Tafsiri ya *Things Fall Apart* (Achebe, 1958)

Tangu mwanzoni mwa miaka ya sabini wafasiri wengine Waafrika waliona umuhimu mkubwa wa kuongeza fasihi ya kisasa ya nchi za Afrika katika idadi ya tafsiri za kifasihi za Kiswahili. Miongoni mwao ni Clement Ndulute, aliyekuwa mhadhiri wa Fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati huo², aliyeamua kutafsiri kwa Kiswahili riwaya mashuhuri sana ya Kiafrika iliyoandikwa kwa Kiingereza nchini Nigeria, yaani *Things Fall Apart* ya Chinua Achebe.

Mhusika mkuu wa kazi hii ni Okonkwo aliyefuata mila na desturi za Kiigbo vizuri sana ili kumshinda baba yake ambaye alikuwa duni na hakuheshimiwa katika jamii yake. Siku moja Okonkwo kwa bahati mbaya alimuua mwanakijiji mwingine na akahukumiwa kuondoka kijijini kwake kwa miaka saba. Huko uhamishoni Okonkwo alikutana na wamishonari Wazungu, na baba yake alisikitika sana kugundua kuwa mwanawe alikubali dini ya Kikristo. Okonkwo aliporudi kijijini baadaye alikuta hata maisha ya kijijini yameathiriwa na hiyo dini mpya. Alianza kuupiga vita Ukristo, hatimaye aliona kuwa haiwezekani kurudi nyuma kwa maisha ya kimila akajiua kwa kujinyonga. Riwaya hiyo inianza na maneno yafuatayo:

Okonkwo was well known throughout the nine villages and even beyond. His fame rested on solid personal achievements. As a young man of eighteen he had brought honour to his village by throwing Amalinze the Cat. Amalinze was the great wrestler who for seven years was unbeaten, from Umofia to Mbaino (uk. 3).

Okonkwo alijulikana katika vijiji vyote tisa na hata nje ya vijiji hivyo. Sifa yake ilitokana na mafanikio yake imara. Alipokuwa na umri wa miaka kumi na minane alikiletea heshima kijiji chake kwa kumtupa mweleka Amalinze, aliyefahamika kama Paka. Amalinze alikuwa ndiye shujaa wa kupiga mieleka ambaye kwa miaka saba hakuwa ameshindwa na mtu (uk. 7).

Mfano huu unaonesha jinsi mtindo wa kutafsiri wa Ndulute ulivyo tofauti sana na ule wa Kawegere. Ndulute “amenakili” (msamiati uliotumiwa na Hermans, 1988, na Lincoln 2006)³ majina ya wahusika (Okonkwo, Amalinze n.k.) na kwa jumla

² Siku hizi anaishi Marekani na ni Profesa wa Kiingereza na Fasihi Linganishi katika Chuo Kikuu cha Tuskegee.

³ Wataalamu hawa waliainisha mikakati mbalimbali ya kutafsiri majina ya wahusika wa kifasihi, miongoni mwao: “to copy” (kunakili), yaani kutobadilisha hata kidogo majina ya kigeni; “to

aliambatana sana na matini chanzi. Mfasiri aliamua kutafsiri kazi hii ya fasihi kwa kuhifadhi kipengele muhimu cha kisanii kinachotumiwa na mwandishi wa matini chanzi, yaani tabia ya kuingiza maneno ya lugha ya Kiigbo wakati anaandika kwa Kingereza. Kwa mujibu wa wahakiki wengi, miongoni mwao Paul Bandia (2014), waandishi Waafrika wanaoandika kwa lugha za kigeni zilizoingia barani Afrika wakati wa ukoloni wanaweza kutazamwa kwa kiasi fulani kama wafasiri. Hii inatokana na sababu kwamba waandishi hao wanapokuwa wakibuni kazi zao huwa wanafikiri kwa lugha mbili au zaidi na mara nyingi wanajitahidi kutafsiri maneno yao ya kitamaduni kwa lugha ya kigeni, au mara nyingine wanaona bora kutumia msamiati kutoka lugha ya Kiafrika ambao huelezwa katika sherehe au katika matini yenyewe. Kwa kufuata mtazamo huu, tafsiri za Kiswahili za kazi za fasihi ya Kiafrika zilizoandikwa kwa lugha za kigeni zinaonekana kidogo kama “tafsiri za tafsiri”. Ndiyo maana tafsiri ya Ndulute haikubadilisha majina ya wahusika wala ya vijiji (Umuofia, Mbaino, Mbanta, nk), ya miungu yao (*Ani, Chi, Ifejioku*, nk), na ya vitu vya utamaduni wao kwa mfano vyombo vya muziki (*ekwe, udu, ogene*, nk). Aidha, hakutafsiri kwa Kiswahili salamu (“*Umuofia kwenu*” na jibu lake “*Yaa!*”) na maneno mengi ya kitamaduni.

Kwa hakika kazi ya mfasiri ilisaidiwa na mtindo wa mwandishi mwenyewe, ambaye mara kwa mara anaingiza maelezo ya vipengele vya utamaduni wa Waigbo katika maandishi, kama katika mfano ufuatao:

*... even now he still remembered how he had suffered when a playmate had told him that his father was **agbala**. That was how Okonkwo first came to know that **agbala** was not only another name for a woman, it could also mean a man who had taken no title* (uk. 13).

Aliweza kukumbuka jinsi alivyoumizwa moyo wakati mwenzi wake aliposema Unoka, baba ya Okonkwo, alikuwa **agbala**. Wakati huo ndipo alifahamu kuwa **agbala** haikuwa na maana mwanamke tu, bali hata mwanamume, ambaye hakuwahi kupata jina la heshima (uk. 19).

Kwa nadra sana mfasiri anafuata mkakati wa kupunguza vipengele vya utamaduni vya matini chanzi kwa kuingiza maneno ya kijumla mahali pa maneno ya kitamaduni ya Waigbo, kwa mfano katika ukurasa 73 ambapo “*black patterns drawn with uli*” (mapambo meusi yaliyochorwa na *uli*, yaani mmea fulani wenye mbegu zinazotia rangi, uk. 66) zimekuwa “*mapambo ya kupendeza*” tu.

Kwa ujumla Ndulute anahifadhi kwa kiwango kikubwa vipengele vya lugha na utamaduni wa Waigbo, ambavyo vitaonekana kama vigeni kwa wasomaji wa lugha lengwa, yaani Kiswahili. Kwa namna hiyo mfasiri anafanya wasomaji wa

transcribe/transliterate” (kunukuu kwa mfumo tofauti), yaani kurekebisha kidogo majina kwa kufuata maumbo ya lugha lengwa; “to substitute” (kuweka badala ya), yaani kutumia majina tofauti kabisa na yale ya matini chanzi (tz. Hermans 1988: 12-13 na Lincoln 2006: 50-52).

Afrika Mashariki wajue zaidi juu ya maisha ya Waigbo, jamii kutoka Afrika Magharibi, kulingana na mawazo ya kukuza Muungano wa Waafrika, ambayo yalipamba moto katika miaka ya sabini baada ya kusisitizwa sana na K. Nkrumah, J. Nyerere na wengineo wengi. Mfasiri haongezi maelezo au tanbihi yoyote katika tafsiri yake, kwa hivyo maneno mengi ambayo hayajaelezwa katika matini chanzi hayaeleweki kabisa kwa wasomaji lengwa (kwa mfano nyimbo kadhaa za Kiigbo).

Isitoshe, mfasiri alichagua kukazia zaidi hali ya afrikanaizesheni ya riwaya hii kuliko mtungaji asili. Kwa sababu hiyo, aliamua kubadilisha kichwa cha kitabu hiki, *Things fall apart* (Mambo yanaparaganyika), maneno yanayotokana na shairi liitwalo “*The Second Coming*” la William Yeats, mtungaji wa mashairi ya Kiingereza kutoka Ayalandi. Ndulute alifuta dondoo hii ya fasihi ya Kiingereza na mahali pake aliandika *Shujaa Okonkwo* kwa ajili ya kuvuta macho ya wasomaji wa Kiswahili juu ya hadithi ya mhusika mkuu Mwafrika.

Ingawa kimsingi mtindo wa kutafsiri wa Ndulute ni tofauti sana na ule wa Kawegere, kwa kuwa mfasiri huyu aghalabu anaambatana sana na matini chanzi, hata hivyo mwishoni mwa riwaya hata yeye anaingiza ubunifu bila kujali kusudio la mwandishi asili. *Things fall apart* inamalizika kwa maneno haya:

He [the District Commissioner] had already chosen the title of the book, after much thought: The Pacification of the Primitive Tribes of the Lower Niger (uk. 187).

Bwana D. C. alikuwa amekwisha chagua jina la kitabu hicho baada ya taamuli kubwa: Uletaji sulubu kwa washenzi wa mto Niger (uk. 194).

Kwa kuandika “uletaji wa sulubu” badala ya “uletaji wa amani” walivyofanya wafasiri wengine, miongoni mwao mfasiri wa Kifaransa na mfasiri wa Kidachi⁴, Ndulute ameondoa kejeli iliyotumiwa na Chinua Achebe akiwa anawasilisha mawazo ya kiuongo ya mkoloni.

2.3 Mzee na Bahari (Tirumanywa, 1980) Tafsiri ya *The Old Man and the Sea* (Hemingway, 1952)

The Old Man and the Sea ni riwaya ya mwandishi Mmarekani Ernest Hemingway. Mhusika mkuu ni mvuvi mzee sana, Santiago, ambaye anaishi peke yake katika kisiwa cha Cuba akiwa anasaidiwa na kijana mmoja, Manolin. Lakini siku moja kwa kuwa Santiago hakunasa samaki kwa siku nyingi, wazazi wa Manolin walikataa kuendelea kufanya kazi pamoja. Santiago alikwenda baharini mbali sana bila msaidizi yeyote, akavua samaki mkubwa zaidi ya chombo chake. Kwa hiyo alimwacha nje ya chombo na alitumia nguvu zake zote kumvuta mpaka aliporudi

⁴ M. Ligny, mfasiri wa Kifaransa, aliandika “La Pacification des Tribus primitives du Bas-Niger” (1983, uk. 254). Mfasiri wa Kidachi D. Heusler alitafsiri “Beiträge zur Befriedung der Eingeborenenstämme im Gebiet des Unteren Niger” (1983, uk. 210).

bandarini. Hapo alitambua kwamba samaki wengine walikuwa wamekwishakula sehemu nyingi za mwili wa kiumbe aliyevuliwa naye. Sehemu ya kwanza ya kitabu hicho inasema:

He was an old man who fished alone in a skiff in the Gulf Stream and he had gone eighty-four days now without taking a fish. In the first forty days a boy had been with him. But after forty days without a fish the boy's parents had told him that the old man was now definitely and finally salao, which is the worst form of unlucky, and the boy had gone at their orders in another boat which caught three good fish the first week (uk. 5).

Alikuwa Mzee mvuvi, aliyevua peke yake mtumbwini katika Mkondo Mkuu, Bahari la Atlanta. Kwa siku themanini na nne alikuwa hakuambulia chochote. Siku arobaini za kwanza, alikuwa pamoja na mtoto mvulana. Lakini baada ya siku arobaini bila mafanikio, wazazi wa Mtoto walimwambia kwamba Mzee alikuwa bila shaka **salao**, yaani mtu wa shari. Kwa maagizo yao, Mtoto aliingia katika mtumbwi mwingine; nao ulinasa samaki watatu wakubwa, juma la kwanza (uk. 1).

Mfano huu unaanza kudhihirisha mtindo wa mfasiri Tirumanywa, ambaye ni padri na mtaalamu wa Biblia kutoka jimbo kuu la Mwanza. Tirumanywa hakutafsiri kitabu hiki kwa kuhamisha vipengele vyake vya kigeni bali alitaka wasomaji wa Kiswahili wakabiliane na mandhari na jamii mpya, yaani kisiwa cha Kuba, ambapo mwandishi Hemingway aliishi kwa siku nyingi. Hata hivyo Tirumanywa, kwa namna tofauti na ile ya Ndulute, wakati fulani anaongeza maelezo kwa ajili ya wasomaji wa lugha lengwa. Mathalani, katika nukuu ya hapo juu anaingiza taarifa kuwa Mkondo mkuu umo katika Bahari ya Atlanta. Aidha, wakati fulani mfasiri huyu haogopi kubadilisha miundo ya sentensi katika matini chanzi, yamkini ili mtiririko wake ukaribiane zaidi na lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, katika dondoo ya hapo juu sentensi ya tatu ya matini chanzi ambayo ni ndefu kidogo iligawanywa na Tirumanywa na kuwa sentensi mbili katika tafsiri ya Kiswahili.

Aidha, Tirumanywa hakubadilisha mtindo wa uandishi wa Hemingway, ambaye ametumia sana maneno ya Kiispania, si kwa kuchora mandhari ya nchi ya kigeni tu, bali kwa kueleza vipengele vingi vya lugha na utamaduni vya jamii ya Kuba. Kwa hivyo, mfasiri hakutafsiri kwa Kiswahili maneno hayo, kama katika mifano inayofuata:

*The shack was made of the tough bud-shields of the royal palm which are called **guano** (uk. 8).*

Kibanda chenyewe kilikuwa kimejengwa kwa makuti ya mivaa, ijulikanayo kama **guano** (uk 6).

*He always thought of the sea as **la mar** which is what people call her in Spanish when they love her. Sometimes those who love her say bad things of her but they are always said as though she were a woman. Some of the younger fishermen, those who used buoys as floats*

*for their lines and had motorboats, bought when the shark livers had brought much money, spoke of her as **el mar** which is masculine. They spoke of her as a contestant or a place or even an enemy* (k. 19-20).

Aliita bahari daima **la mar**, yaani jina la kike kama waitavyo watu kwa Kispania, kuonyesha ubembe. Pengine wale wanaoipenda, husema mabaya juu yake, kama ambavyo wangesema juu ya mwanamke. Baadhi ya vijana wavuvi waliita bahari jina la kiume, **el mar**. Hawa ndio waliotumia chelezo na mitumbwi ya injini, baada ya kutajirika kwa kuuza maini ya papa. Walifikiria bahari kama mshindaji, au kama uwanja, au hata kama adui. (uk. 17)

Katika nukuu hii mabadiliko ya jinsia ya kisarufi ya Kiispania⁵ yanaakisi mgogoro baina ya wazee na kizazi kipya kuhusu jinsi ya kuhusiana na bahari na hayatafsiriki kabisa kwa Kiingereza wala kwa Kiswahili. Kama ilivyoonekana katika dondoo ya kwanza, Tirumanywa alihifadhi kwa kiasi kikubwa vipengele vya utamaduni vya matini chanzi, isipokuwa wakati fulani anaviasilisha kidogo kwa mbinu nyingi zikiwamo:

- Majina ya watu hayakubadilishwa, ila yamerekebishwa kidogo ili kufuata matamshi ya Kiswahili. Kwa mfano, jina la Manolin limekuwa Manolino. Mkakati huu unakumbusha mtindo wa J. Nyerere katika tafsiri yake ya tamthilia za Shakespeare, ambapo jina la Julius Caesar limekuwa Juliasi Kaizari, jina la Portia limeandikwa Poshia, n.k.
- Majina ya baadhi ya vyakula yanaelezwa, kwa mfano tafsiri ya “*yellow rice*” ni “wali wa bizari”.
- Mambo kadha ya kitamaduni yamebadilishwa kuwa ya kawaida ya Afrika Mashariki. Kwa mfano sentensi ya “*I have yesterday’s paper and I will read the baseball*” (uk. 10) imetafsiriwa “Nina gazeti la jana, na nitasoma habari za mpira” [ingawa Tirumanywa aliacha majina ya timu za besiboli za Marekani (Yankees na Indian of Cleveland) na jina la bingwa mwenye asili ya Italia Joe Di Maggio, anayependwa sana na washabiki Wamarekani wa mchezo huu].

Hatimaye, Tirumanywa katika tafsiri yake ya riwaya ya *Old man and the sea* hakubuni tena aya fulani za matini chanzi kama walivyofanya wakati mwingine Kawegere na Ndulute bila kujali sana makusudio ya kimaana ya mwandishi. Hata hivyo, tafsiri yake ambayo imeviasilisha kidogo vipengele vya utamaduni vya matini chanzi imefanikiwa kukaribia hadhira ya wasomaji wa Afrika Mashariki

⁵ Katika Kiispania, Kiitaliano na lugha nyingine zinazotokana na Kilatini, hakuna mfumo wa ngeli za nomino kama katika lugha za Kibantu. Majina yanatofautiana katika vikundi viwili vya kisarufi, yaani majina ya kike na ya kiume.

ambao wataweza kuelewa mafumbo ya matini chanzi na kuyahusisha na muktadha wa jamii yao.

2.4 Jambo la Maana (Hussein, 1982) tafsiri ya hadithi tatu za Hans Christian Andersen: *The Emperor's New Clothes* (Nguo Mpya za Mfalme, 1837), *Something* (Jambo la maana, 1858) na *The Old Street Lamp* (Taa ya Zamani ya Barabarani, 1847)

Hadithi fupi hizi zimetungwa na Hans Christian Andersen, mwandishi Mdenish, kwenye karne ya kumi na tisa. Mtungaji aliziandika kwa Kidenish, baadaye zilizopendwa zaidi zikatafsiriwa kwa lugha nyingi za ulimwengu. Mfasiri Ebrahim Hussein, mtunzi mashuhuri wa tamthilia na mashairi nchini Tanzania, kwa kuwa hajui Kidenish lakini anajua vizuri Kidachi na Kiingereza, bila shaka alitumia tafsiri moja kama matini asili. Katika utangulizi wa kitabu hicho hapaelezwi lugha chanzi ya tafsiri ni ipi; hata hivyo tunaweza kuchukulia kuwa mwandishi huyo alitafsiri kutoka Kiingereza, kutokana na maneno fulani ya kigeni yalivyohifadhiwa katika matini ya tafsiri, kama kwa mfano “Hurrah” (uk.12) na “ballet” (uk. 18), ambayo ni maneno ya Kiingereza.

Hadithi ya kwanza inasimulia habari ya mfalme mkuu ambaye alipenda sana nguo nzuri. Siku moja wanafiki wawili walimdanganya kwa kumwambia kuwa wanaweza kufuma nguo yenye sifa ya kutoonekana kwa mtu yeyote yule aliyekuwa haifai kazi yake au aliyekuwa mjinga. Waziri na watu wote walijifanya kuiona nguo hiyo kwa sababu hawakutaka kuonekana kama wajinga. Hatimaye mfalme huyo akajikuta kwenye maandamano akiwa uchi na hakuna mtu anayethubutu kusema ukweli ila mtoto mdogo tu. Hapo mfalme aliona aibu sana lakini aliendelea kutembea kwa maringo.

Hadithi ya pili inahusu ndugu watano waliotaka kufanya jambo la maana. Ndugu mkubwa alikuwa mtengenezaji wa matofali, wa pili mwashi, wa tatu mjenzi, wa nne mvumbuzi, na wa tano mhakiki. Halafu wote walikufa, na yule wa tano akajikuta mstarini kwa kuingia peponi pamoja na bibi kizee ambaye aliruhusiwa ndani kwa kuwa aliokoa watu wengi. Alipoona kuwa kimbunga kitavunja barafu ambapo wananchi walikuwa wakistarehe, aliwasha moto nyumba yake ili waondoke huko kwenda kwake. Wote wakawa salama lakini bi kizee akafariki kwa baridi. Malaika alipotaka kumrudisha mhakiki duniani kwa kuwa hakufanya lolote, bibi yule alimwomba akisema kuwa alisaidiwa kujenga na nduguye mtengeneza matofali. Malaika alikubali mhakiki akae nje mpaka atende jambo jema. Wakati alipokuwa akiwaza kwamba yeye angeweza kuongea vizuri zaidi kuliko Malaika, mhakiki kwa mara ya kwanza alifanya jambo la maana, yaani kukaa kimya.

Hadithi ya tatu ni kuhusu taa ya zamani ya barabarani iliyoambiwa kuwa siku inayofuata watu wa Baraza Kuu la Jiji watakata shauri ikiwa inaweza

kuendelea na huduma yake au la. Taa iliogopa sana kuwa itaondolewa na labda itayeyushwa kwa kutengeneza kifaa kingine. Aidha ilisikitika kutengana na askari wa usiku na mkewe ambao walikuwa kama familia yake. Kwa bahati nzuri askari na mkewe waliopenda sana taa ile waliamua kuichukua nyumbani kwao na kuitunza vizuri.

Katika makala hii nitajikita zaidi juu ya hadithi ya kuchekesha ya *Nguo Mpya za Mfalme*. Tuangalie jinsi mfasiri alivyotafsiri mwanzo wake:

Many, many years ago there was an emperor who was so terribly fond of beautiful new clothes that he spent all his money on his attire. He did not care about his soldiers, or attending the theatre, or even going for a drive in the park, unless it was to show off his new clothes. He had an outfit for every hour of the day. And just as we say, "The king is in his council chamber", his subjects used to say, "The emperor is in his clothes closet" (uk. 77).

Hapo kale palikuwa na mfalme aliyekuwa anapenda sana nguo nzuri mpya. Alitumia pesa zake zote katika mavazi yake. Alibadilisha mavazi kila baada ya saa moja. Hakuwajali askari wake. Hakujali kutazama michezo ya kuigiza wala kutembea bustanini na gari lake la farasi. Na alipofanya hivyo basi, ilikuwa kwa ajili ya kuonyesha nguo zake mpya kwa watu. Kama tunavyosema "Mfalme yumo katika chumba chake cha halmashauri" watu walikuwa wanasema "Mfalme yumo katika chumba chake cha nguo!" (uk.1)

Kwanza tuzingatie kuwa, tofauti na riwaya zilizochambuliwa hapo juu, matini asili ya Andersen haielezi bayana muktadha wa hadithi (ni wakati gani, nchi gani), wala haitaji majina ya wahusika. Hussein hakubadilisha mtindo huu ambao ni wa kawaida kwa hadithi nyingi za kijadi za kiulaya, unafanana sana na baadhi ya masimulizi ya Kiafrika.

Mwandishi huyo hafuati mkakati mmoja wa tafsiri peke yake kama inavyoonekana katika dondoo ya mwanzo wa hadithi. Kwa upande mmoja anaegemea matini asili na anahifadhi baadhi ya vipengele vyake ambavyo ni vigeni kwa hadhira lengwa. Tafsiri yake ya "*going for a drive in the park*", yaani "kutembea bustanini na gari lake la farasi", si tafsiri ya kijuujuu, bali inaeleza vizuri maana ya sentensi hii ili wasomaji wa Kiswahili wapate taarifa ya tabia ya wazungu wa zamani ya kutembea na gari linalovutwa na farasi.

Kwa upande mwingine, Hussein anaasilisha kidogo hadithi hii kwa kutumia mbinu mbalimbali. Kwa mfano, mfasiri ametafsiri "emperor" na "king" kwa msamiati ule ule wa Kiswahili, yaani "mfalme", hata kama neno "emperor" linamaanisha mfalme mkuu ambaye anatawala nchi nyingi. Aidha, kama inavyoonekana vizuri katika dondoo la hapo juu, mfasiri anabadilisha namna sentensi zilivyotengwa katika matini chanzi ili ziwe fupi fupi. Kwa namna hiyo, mtiririko wa hadithi hii umekuwa mwepesi zaidi kuliko ule wa matini chanzi. Aidha, aliamua kubadilisha kidogo mpangilio wa aya hii na kuhamisha mahala pengine sentensi ya "*He had an outfit for every hour of the day*".

Katika kitabu hiki tunapata mifano mingine ya mtindo wa Hussein, aliyejitahidi kupata ulinganifu mzuri wa mienendo ya kutafsiri. Mfasiri huyo, kama walivyofanya Ndulute na Tirumanywa, hakutaka kuhamisha hadithi hii katika muktadha wa Kiafrika, ili wasomaji wajue vyema kwamba wanakabiliana na fasihi iliyobuniwa Ulaya wakati wa zamani. Kwa hivyo, kama tulivyokwisha sema mfasiri aliamua kutotafsiri maneno machache ya lugha chanzi, hata wakati ingekuwa si vigumu sana kupata kisawe cha Kiswahili, kwa mfano neno la “*hurrah!*” ambalo linaweza kutafsiriwa kwa kutumia milio ya shangwe ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, alihifadhi vipengele vingi vya utamaduni wa kiulaya ambavyo vingekuwa vipya kwa hadhira lengwa na alitafsiri maana zake kwa kutumia msamiati wa Kiswahili. Kwa mfano, neno “*train of the mantle*” limetafsiriwa “mkia wa lile koti” (uk. 6), “*the lords of the bedchamber*” wamekuwa “waheshimiwa wawili kutoka chumba cha kulala cha mfalme” (uk. 7). Tafsiri hii ya mwisho kwa upande mmoja inasaidia wasomaji kupata picha ya jinsi waheshimiwa wa enzi zile za Ulaya walivyokuwa wanamfuata mfalme huku wakichukua mapindo mawili ya mkia wa koti lake. Kwa upande mwingine, mfasiri haongezi maelezo kuwa tafsiri hii sisizi “waheshimiwa kutoka chumba cha kulala cha mfalme” ni jina la heshima la kizungu kwa watu wenye cheo kikubwa. Kadhalika, mfasiri aghalabu anahifadhi vitu vya utamaduni vya matini bila kuviasilisha, kama kwa mfano fungu la maneno “*a large colored print, representing the congress of Vienna*” limetafsiriwa “picha kubwa ya Baraza Kuu la Jiji la Vienna” (*Taa ya zamani ya Barabarani*, uk.25).

Hata hivyo mfasiri aliwajali pia wasomaji wa lugha lengwa na alitaka kuasilisha kwa kiasi fulani kazi hii ya fasihi. Kwa mfano, katika tafsiri yake ya hadithi ya “*Something*”, Hussein alihifadhi jina la mhusika *Margaret* lakini alilirekebisha kidogo, kama ambavyo alifanya Tirumanywa na kabla yake J. K. Nyerere, kwa kutumia matamshi ya Kiswahili na majina ya heshima ya Kiswahili, liwe Mama Margreta au penginepo Bi Kizee Margreta. Isitoshe, baada ya kutaja Mama Margreta mfasiri aliongeza sentensi fafanuzi katika matini ya tafsiri yake, yaani “Mama” ni jina ambalo watu masikini waliwapa wanawake wazee waliowapenda” (uk. 11), ili kuwaeleza wasomaji matumizi ya jina hilo la heshima katika kazi hii ya fasihi ya kigeni. Aidha, mfasiri wakati fulani anaongeza kiingizi kwenye matini ya tafsiri (kwa mfano “Lo!”, *Nguo Mpya za Mfalme* uk.79), au anatafsiri baadhi ya semi za kitabu hicho kwa kuzihamisha kwenye utamaduni wa Kiswahili. Mathalani, msemu “*God preserve me!*” (*Nguo Mpya za Mfalme* uk. 78) ilitafsiriwa “Mungu wangu, rabi salama!” (uk. 2).

Juu ya yote, namna yake ya kuasilisha matini hii ya kigeni inahusu kiwango cha uandishi, kwa kuwa katika kitabu hiki mfasiri Hussein alibadilisha sana jinsi sentensi zilivyotengwa na zilivyopangiliwa katika matini chanzi, kama tulivyoona

hapo juu, tena yeye alibadilisha jinsi sentensi zilivyounganishwa, kama mfano ufuatao unaopatikana mwishoni mwa hadithi hii unavyoonesha:

“He has nothing on!” shouted all the people at last. The emperor shivered, for he was certain that they were right; but he thought, “I must bear it until the procession is over.” And he walked even more proudly, and the two gentlemen of the imperial bedchamber went on carrying the train that wasn’t there (uk. 81).

Hatimaye watu walipiga kelele, “Yuko uchi.” Lakini Mfalme aliposikia hivyo alitetemeka mwili mzima, kwani alijua wazi kwamba maneno hayo ni ya kweli. “Lazima niendeleo mpaka maandamano yamalizike.” Na alitembea kwa maringo zaidi, na wale waheshimiwa wawili kutoka chumba cha kulala cha mfalme waliendelea kuuchukua mkia wa koti ambao haukuwepo (uk. 7).

Hapo juu mfasiri aliondoa maneno ya kiungo “*but he thought*” (lakini alifikiri) ambayo katika matini chanzi yanatanguliza fikra ya mfalme, kwa hivyo katika tafsiri fikra hiyo hiyo inawafikia wasomaji moja kwa moja. Kwa sababu maneno ambayo Mfalme anayafikiri hayatangulizwi na sauti ya msimuliaji.

3.0 Hitimisho

Tumeona kuwa baada ya ukoloni baadhi ya waandishi Watanzania walitambua umuhimu wa kutafsiri fasihi ya kigeni kwa Kiswahili, kwanza kwa kuonyesha uzuri wa lugha ya Kiswahili, pia kwa kukuza idadi ya maandishi ya kisasa ya Kiswahili. Shughuli ya tafsiri ya kifasihi imezingatiwa kwa upande wa maandishi ya kinathari, kwa ajili ya kuanza kufafanua jinsi wafasiri Watanzania walivyotafsiri kwa Kiswahili baadhi ya hadithi na riwaya za kigeni. Makala hii ilichambua baadhi tu ya kazi za tafsiri ya Kiswahili. Kazi zilizoambuliwa ni: *Shamba la Wanyama* (tafsiri ya *Animal Farm* ya G. Orwell) iliyotafsiriwa na Fortunatus Kawegere, *Shujaa Okonkwo* (tafsiri ya *Things fall apart* ya C. Achebe) iliyotafsiriwa na Clement Ndulute, *Mzee na Bahari* (tafsiri ya *The Old man and the sea* ya E. Hemingway) iliyotafsiriwa na Cyprian Tirumanywa, na *Jambo la Maana* (tafsiri ya hadithi tatu za H. C. Andersen) iliyotafsiriwa na Ebrahim Hussein.

Kazi hizo zote zilitafsiriwa kutoka Kiingereza, hata hadithi tatu za H. C. Andersen zilizoandikwa awali kwa lugha nyingine, yaani Kidenish. Mwenendo huu ni mpana sana nchini Tanzania, hata siku hizi wafasiri wanaendelea kutafsiri fasihi ya kigeni wakiegemea karibu mara zote katika matini zilizoandikwa au zilizofasiriwa kwa Kiingereza. Tabia hii inaweza kuhusishwa na ukweli kwamba nchini Tanzania lugha za kigeni ambazo si Kiingereza bado hazijafundishwa sana katika masomo ya juu.⁶

⁶ Mifano ya “tafsiri za tafsiri” ni *Barua ndefu kama hii*, tafsiri ya riwaya ya *Une si longue lettre* ya mwandishi mwanamke Msenegali Mariama Bâ, iliyoandikwa kwa Kifaransa na iliyotafsiriwa toka Kiingereza na marehemu Clement Maganga (1994), na *Msako*, tafsiri ya *Al-Tariq* ya mwandishi

Katika uchambuzi wa tafsiri hizi nilijikita katika utofautishaji wa mikakati miwili ya kitafsiri, yaani ama kuambatana sana na matini chanzi na kuhifadhi vipengele vyake vingi vya lugha na utamaduni, au kuhamisha matini chanzi kwenye lugha na utamaduni wa lugha lengwa. Mifano iliyotolewa katika makala hii imeonesha kuwa kuna njia nyingi ya kuhawilisha vipengele vya utamaduni vya matini chanzi kwenda lugha lengwa. Kawegere ndiye aliyehamisha zaidi matini asili kwenye utamaduni wa lugha lengwa ili wasomaji wa Kiswahili waisome kama hadithi ya kienyeji kabisa. Wafasiri wengine, kila mmoja na mtindo pekee ukiathiriwa na mtazamo wake wa kiitikadi na wa kisanii, walijitahidi kupata ulinganifu fulani baina ya kuhifadhi maana na vipengele vingi vya utamaduni wa kigeni vya matini chanzi na wakati mmoja kuwataarifu wasomaji wa lugha lengwa kufuatana na mazingira yao yenyewe.

Marejeleo

- Achebe, C. (1996/1958). *Things Fall Apart*. London: Heinemann.
- Haugaard, E. (mfasiri). (1976). *Hans Andersen: His Classic Fairy Tales*. London: Linx.
- Bandia, P. (2014). *Translation as Reparation. Writing and Translation in Postcolonial Africa*. New York: Routledge.
- Bertoncini Zúbková, E. na wenzake. (2009). *Outline of Swahili Literature*. Leiden: Brill.
- Eco, U. (2003). *Dire quasi la stessa cosa*. Milano: Bompiani.
- Havelaar” katika M. J. Wintle (mhariri) *Modern Dutch Studies. Essays in Honour of Professor Peter King on the Occasion of his Retirement*. London/Atlantic Highlands: The Athlone Press.
- Hemingway, E. (1977/1952). *The Old Man and the Sea*. New York: Scribners.
- Hermans, T. (1988). “On Translating Proper Names, with Reference to De Witte and Max Heusler, D. (mfasiri). (1983). *Okonkwo oder Das Alte stürzt*. Frankfurt/Main: Surhkamp Verlag.
- Hussein, E. (mfasiri). (1982). *Jambo la Maana*. Dar es Salaam: Africana Publishers.
- Kawegere, F. (mfasiri). (1967). *Shamba la Wanyama*. Nairobi: East African Publishing House.
- Ligny, M. (mfasiri). (1983). *Le monde s’effondre*. Paris: Présence Africaine.
- Lincoln, F. 2006. "Translation of Names in Children's Fantasy Literature: Bringing the Young Reader into Play." *Translation Studies* Na. 2, kur. 44-57.
https://www.researchgate.net/publication/237246131_Translation_of_Names_in_Children's_Fantasy_Literature_Bringing_the_Young_Reader_into_Play_i, imesomwa tarehe 9 Septemba 2016.
- Maganga, C. (mfasiri). (1994). *Barua Ndefu kama Hii*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

- Mazrui, A. (2007). *Swahili Beyond the Boundaries: Literature, Language, and Identity*. Athens: Ohio University Press.
- Mwansoko, H. J. M. na wenzake. (1996). *Kitangulizi cha Tafisiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Ndulute, C. (mfasiri). (1973). *Shujaa Okonkwo*. Nairobi: East African Publishing House na Heinemann Educational Books (East Africa).
- Nyerere, J. K. (mfasiri). (1969). *Juliasi Kaizari*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Nyerere, J. K. (mfasiri). (1969). *Mabepari wa Venisi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character, and Continuity*. USA: Indiana University Press.
- Orwell, G. (1987/1945). *Animal Farm*. London: Penguin Books.
- Ruhumbika, G. 1983. "Tafisiri za Fasihi za Kigeni katika ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili", *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*, Dar es Salaam: TUKI, kur. 253-266.
- Simba, D. M. (mfasiri). (2004). *Msako*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Tirumanywa, C. (mfasiri). (1980). *Mzee na Bahari*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Venuti, L. (1995). *The Translator's Invisibility: A History of Translation*. London/ New York: Routledge.
- Wamitila, K. W. (1999). "What's in a Name: Towards Literary Onomastics in Kiswahili Literature", *Swahili Forum*, 35-44.
- Wamitila, K. W. 2003. *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Focus Publications.